# Kufifia kwa Lahaja za Kiswahili katika Karne ya 21: Mfano wa Lahaja ya Kimakunduchi

*Zainab Ali Iddi*
*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza mambo yanayochangia kufifia kwa lahaja za Kiswahili katika karne ya 21 kwa kutumia lahaja ya Kimakunduchi ya Kusini Unguja, kama mfano mahsusi. Lahaja hii, mojawapo ya lahaja kongwe za Kiswahili, imekuwa sehemu muhimu ya utambulisho, urithi na historia ya jamii ya Wamakunduchi. Lakini kwa sasa inakabiliwa na tishio kubwa la kupotea kutokana na sababu mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na kisera. Hoja kuu za makala zinajikita katika athari za upendeleo wa Kiswahili Sanifu katika mifumo rasmi kama vile elimu, utawala na vyombo vya habari, hali inayosababisha jamii kuitazama lahaja yao kama lugha duni au isiyo rasmi. Aidha, makala imeeleza namna mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, ikiwemo uhamiaji, ndoa mseto na maendeleo ya kiteknolojia, vinavyochangia vijana kuachana na matumizi ya Kimakunduchi katika mazingira ya nyumbani na kijamii. Aidha, makala imejikita katika uchambuzi wa kina kwa kutumia *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972), ambayo inafafanua mahusiano baina ya mazingira ya kijamii na ustawi au kufifia kwa lahaja. Pia, taarifa kutoka tafiti ndogo zilizofanyika Zanzibar zinathibitisha mwenendo wa kupungua kwa idadi ya wazungumzaji vijana wa Kimakunduchi, jambo linalodhihirisha hali mbaya ya lahaja hiyo. Makala inapendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuhifadhi na kuhuisha lahaja ya Kimakunduchi, ikiwemo kuweka sera madhubuti za elimu na utamaduni, kutumia teknolojia katika kuandaa maandiko na rekodi za lahaja, pamoja na kushirikisha jamii na wazee wenye ufasaha katika ufundishaji na uhamasishaji wa matumizi ya lahaja hiyo kama sehemu muhimu ya urithi na utambulisho wa Zanzibar.**

**Maneno Muhimu:** *Lahaja, Kiswahili, Karne ya 21, Kimakunduchi, Elimu, Utamaduni, Teknolojia*

## Utangulizi

Lugha ni kielelezo muhimu cha utambulisho wa jamii na lahaja ni tanzu za lugha zinazochangia utajiri wa mawasiliano, historia na utamaduni wa jamii inayohusika. Lahaja huakisi tofauti za kijiografia, kijamii na kihistoria za wazungumzaji wake, hivyo kuwa msingi muhimu katika kuelewa mienendo na uhusiano ndani ya jamii. Katika mazingira ya lugha ya Kiswahili, lahaja zimekuwa zikichukua urithi wa kipekee wa utamaduni na historia, zikionyesha tofauti za maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, pamoja na Kiswahili kuwa lugha rasmi, ya kitaifa na kimataifa, lahaja zake zimeanza kupungua kwa kiasi kikubwa katika matumizi ya kila siku na hata katika mazingira rasmi.

Katika makala haya, tunajikita katika kuchunguza sababu zinazochangia kufifia kwa lahaja za Kiswahili katika karne ya 21 kwa kutumia lahaja ya Kimakunduchi ya Zanzibar kama mfano mahsusi. Kwa mujibu wa watafiti Nurse na Hinnebusch (1993), lahaja ya Kimakunduchi imeathiriwa pakubwa na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali, zikiwemo za Waarabu, Waajemi na Wabantu. Upekee huu wa kihistoria na kiutamaduni unafanya lahaja hii kuwa muhimu katika utafiti wa lugha na utamaduni wa Pwani ya Afrika Mashariki (Massamba, 2017). Hata hivyo, umaarufu na matumizi yake katika jamii yanaendelea kushuka kwa kasi kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kijamii na kiuchumi yanayosababisha lahaja kuu, kama Kiswahili Sanifu, kupendelewa zaidi.

Mazrui na Mazrui (1995) wamebainisha kuwa matumizi makubwa ya Kiswahili Sanifu katika taasisi za elimu, serikali na vyombo vya habari yamechangia kudhoofisha lahaja za kienyeji, kikiwemo Kimakunduchi. Kiswahili Sanifu kimekuwa kikipewa hadhi ya lugha rasmi katika mifumo yote rasmi, hali inayosababisha lahaja za kienyeji kuchukuliwa kama zisizokuwa na thamani katika

maendeleo ya kitaifa na kijamii. Athari za jambo hili zinaonekana zaidi kwa vijana ambao hawapati fursa ya kujifunza wala kutumia lahaja zao katika mazingira rasmi na hata yasiyo rasmi, hivyo kutokuthamini urithi huu muhimu wa kiutamaduni na kihistoria.

Fishman (1991) katika nadharia yake ya upangaji lugha anaeleza kuwa uhai wa lugha yoyote unategemea zaidi uwezo wa kurithishwa kwake kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia matumizi ya kila siku ya nyumbani. Katika muktadha wa Kimakunduchi, mabadiliko katika mitindo ya maisha na mwingiliano mkubwa wa jamii za vijijini na mjini yameathiri pakubwa mchakato huu wa kurithishwa. Familia nyingi zimekuwa zikikosa hamasa ya kutumia lahaja hii nyumbani, hivyo vijana hawapati fursa ya kujifunza na kuzungumza Kimakunduchi kama lugha yao ya kwanza. Hii inapelekea vizazi vipya kukosa uelewa wa kina wa lahaja yao na hatimaye kuchangia katika kufifia kwake kwa kasi kubwa.

Aidha, maendeleo ya kiteknolojia na ongezeko kubwa la matumizi ya mitandao ya kijamii yamekuwa na athari kubwa katika matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi. Vijana wengi wa sasa wanatumia teknolojia hizo kwa mawasiliano ya kila siku, wakipendelea zaidi lugha zinazokubalika kimataifa kama vile Kiingereza au lugha rasmi ya kitaifa kama Kiswahili Sanifu. Kwa mujibu wa ripoti ya UNESCO (2003), lahaja ambayo inapoteza wasemaji wake katika kizazi kipya hupoteza uwezo wake wa kuendelea kuwa hai, hivyo kuingia katika hatari kubwa ya kupotea kabisa. Hivyo basi, matumizi ya teknolojia ya mawasiliano ambayo hayazingatii lahaja za kienyeji yanaongeza kasi ya kupotea kwa urithi huu muhimu wa lugha.

Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza kwa undani sababu zinazoathiri matumizi na uhai wa lahaja ya Kimakunduchi na kutoa mapendekezo mahsusi ambayo yanaweza kusaidia katika juhudi za kuhifadhi na kuhuisha lahaja hiyo. Makala haya yanalenga kuwa chachu kwa jamii, wanataaluma na watunga sera katika kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa lahaja hii muhimu ya Kiswahili haipotei bali inaendelezwa kwa faida ya vizazi vijavyo.

**Maana ya Lahaja na Umuhimu wake**

Lahaja ni aina ya lugha inayozungumzwa katika eneo maalumu au na jamii fulani, ikitofautiana na lugha kuu katika vipengele mbalimbali kama vile matamshi, msamiati, sarufi na matumizi ya misemo maalumu. Kwa mujibu wa wataalamu wa lugha kama vile Crystal (2008), lahaja hutokea kutokana na tofauti za kijamii na kijiografia zinazojitokeza katika jamii yenye wazungumzaji wengi. Lahaja hujenga msingi wa utambulisho wa jamii, zikibeba utajiri mkubwa wa urithi wa kihistoria na kiutamaduni wa eneo au jamii inayohusika. Kwa mantiki hii, lahaja huwa ni kiashiria muhimu cha urithi na uhusiano wa watu wa eneo fulani katika kipindi maalumu cha historia yao.

Katika muktadha wa Kiswahili, Kimakunduchi ni mojawapo ya lahaja kongwe yenye umuhimu wa kipekee kwa jamii ya eneo la Makunduchi, lililoko kusini mwa kisiwa cha Unguja, Zanzibar. Nurse na Hinnebusch (1993) wanabainisha kuwa Kimakunduchi ni zao la mwingiliano wa tamaduni nyingi kama zile za Kiarabu, Kiajemi na Kibantu, jambo linalodhihirisha mseto wa kiutamaduni katika eneo hili. Hali hiyo iliifanya lahaja ya Kimakunduchi kuwa si tu chombo cha mawasiliano, bali pia kama kumbukumbu hai inayodhihirisha mahusiano ya kihistoria ya eneo la Makunduchi na maeneo mengine ya mwambao wa Afrika Mashariki.

Kimakunduchi, kama lahaja nyingine za Kiswahili, hubeba thamani kubwa ya kiutamaduni kutokana na ukweli kwamba kupitia lahaja hii, mila, desturi na maadili mbalimbali ya jamii ya Wamakunduchi hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mdee (2010) anabainisha kwamba lugha ni chombo muhimu cha kuhifadhi maarifa ya jadi na utamaduni wa jamii yoyote ile. Kwa kutumia Kimakunduchi, jamii ya Wamakunduchi imeweza kuhifadhi hadithi, nyimbo, methali na misemo mbalimbali ambayo ni hazina kubwa katika kuelezea na kuelewa historia na utambulisho wao kama jamii.

Aidha, umuhimu wa lahaja hii unatokana na uwezo wake wa kuhifadhi maarifa ya asili kuhusu mazingira, afya na mbinu za maisha ambazo zimekuwa zikisaidia jamii kwa miaka mingi. Kwa mfano, Kimakunduchi kimekuwa kikitumika katika kuelezea aina mbalimbali za mimea ya tiba, mbinu za kilimo na maarifa mengine ya kiasili ambayo ni vigumu kupatikana katika lugha kuu au Kiswahili Sanifu (Iddi, 2011). Hii inaonyesha kuwa lahaja si tu zana ya mawasiliano, bali ni mfumo

wa maarifa muhimu ambao unapaswa kulindwa ili kuhakikisha kwamba maarifa haya ya jadi hayapotei kutokana na kuenea kwa matumizi ya lugha kuu au lugha za kigeni.

Kwa upande mwingine, lahaja kama Kimakunduchi zina umuhimu mkubwa katika utafiti wa kitaaluma, hasa katika nyanja za lugha, fasihi na anthropolojia. Lahaja hii hutumika kama chanzo muhimu cha taarifa za kihistoria na kisayansi kuhusu jamii inayohusika. Kwa mujibu wa Batibo (2005), lahaja zinapokuwa zikitoweka, jamii hupoteza urithi muhimu wa kitaaluma na kihistoria, jambo ambalo linaweza kuwa na madhara makubwa katika tafiti za kitaaluma na katika juhudi za kuelewa mienendo mbalimbali ya jamii zilizopita na zilizopo.

Kwa ujumla, umuhimu wa lahaja ya Kimakunduchi unajidhihirisha katika uwezo wake wa kuhifadhi urithi wa kiutamaduni, kihistoria na kielimu. Jamii ya Wamakunduchi, kama ilivyo kwa jamii nyingine za Kiafrika, ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa lahaja yao inatunzwa na kuendelezwa kwa manufaa ya vizazi vijavyo (Juma, 2018). Hii ni kwa sababu lahaja hii ni sehemu muhimu ya utambulisho wao na ina nafasi kubwa katika kueleza historia na maarifa ambayo hayawezi kupatikana kupitia lugha kuu pekee.

**Mkabala wa Kinadharia**

Makala haya yameongozwa na *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha*[1] ya Einar Haugen (1972), ambayo inaeleza kuwa lugha au lahaja hutegemea mazingira yake ya kijamii, kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia ili kustawi au kufifia. Katika muktadha wa lahaja ya Kimakunduchi, mazingira haya yanajumuisha mifumo ya elimu, sera za lugha, mitazamo ya jamii na maendeleo ya kiteknolojia ambayo kwa pamoja yanaathiri matumizi yake. Kwa mujibu wa Haugen, lugha inaweza kustawi au kuporomoka kutokana na mwingiliano wake na mazingira yake. Matumizi rasmi ya Kiswahili Sanifu katika elimu na vyombo vya habari yamechangia lahaja ya Kimakunduchi kuonekana kama lugha ya chini na hivyo kupoteza thamani yake katika jamii.

Pia, mabadiliko ya kiteknolojia na utandawazi yamesababisha vijana wengi kupendelea lugha zinazokubalika kitaifa na kimataifa kama vile Kiswahili Sanifu na Kiingereza na hivyo kuchangia kupungua matumizi ya Kimakunduchi. Aidha, Haugen anabainisha umuhimu wa sera za lugha katika ukuaji au kudidimia kwa lahaja. Sera za lugha nchini Tanzania na Zanzibar zinazosisitiza matumizi ya Kiswahili Sanifu katika mifumo rasmi zimechangia Kimakunduchi kubaki katika matumizi machache yasiyo rasmi. Kwa ujumla nadharia hii imesaidia kubaini sababu kuu zinazochangia kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi na kutoa mapendekezo ya hatua za kuilinda na kuiendeleza.

**Methodolojia ya Uchunguzi**

Uchunguzi huu ulilenga kubaini sababu zinazochangia kufifia kwa lahaja za Kiswahili kwa kutumia lahaja ya Kimakunduchi kama mfano mahususi. Pia, ulitumia mkabala wa kimaelezo kwa lengo la kupata maelezo ya kina kuhusu hali halisi ya matumizi ya lahaja hii katika jamii ya Wamakunduchi, Zanzibar. Mbinu mbalimbali za ukusanyaji data zilitumika, zikiwemo usaili, majadiliano ya vikundi na uchambuzi wa maandiko mbalimbali yanayohusu sera za lugha na mazingira ya elimu. Data zilikusanywa kati ya Januari na Machi 2025 kutoka vijiji vya Makunduchi, Zanzibar. Sampuli ilijumuisha washiriki 50, wakiwemo wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60, vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 30, walimu kutoka Skuli za Msingi na Sekondari Makunduchi, pamoja na viongozi wa kijamii. Wazee walichaguliwa ili kutoa maelezo kuhusu historia na mabadiliko ya lahaja, wakati vijana walitoa taarifa kuhusu mwenendo wa sasa wa matumizi ya lahaja hiyo.

Majadiliano ya vikundi yalilenga kutambua mitazamo ya jamii kuhusu umuhimu na nafasi ya Kimakunduchi, huku usaili ukisaidia kupata taarifa kuhusu athari za kisera, kielimu na kiteknolojia katika matumizi ya lahaja hii. Maandiko kama vile sera ya lugha, mtaala wa elimu na ripoti mbalimbali za utafiti zilichambuliwa ili kupata taarifa kuhusu sera za lugha zinavyochangia kufifia kwa lahaja hii. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui, ambapo mada kuu zinazochangia kufifia kwa Kimakunduchi zilijadiliwa na kuchambuliwa kwa kina kwa mujibu wa mkabala wa kinadharia wa *Ikolojia ya Lugha* wa Einar

[1] Tafsiri ya "Language Ecology Theory."

Haugen (1972). Uchunguzi huu ulisaidia kubaini sababu kuu za kufifia kwa lahaja hii na kutoa mapendekezo ya hatua madhubuti za kuchukua ili kuihifadhi.

**Mambo Yanayochangia Kufifia kwa Lahaja ya Kimakunduchi**

***Ukuaji na Upendeleo kwa Kiswahili Sanifu***

Mfumo rasmi wa elimu na vyombo vya habari umechangia pakubwa katika kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na matumizi yake ya Kiswahili Sanifu pekee. Katika skuli nyingi za msingi na sekondari Zanzibar, Kiswahili Sanifu ndiyo lugha rasmi ya kufundishia na lahaja za kienyeji kama Kimakunduchi hazina nafasi katika mitaala. Mwalimu mmoja wa Skuli ya Sekondari Makunduchi alieleza:

> Katika skuli yetu, tunatumia Kiswahili Sanifu kwa sababu ndiyo lugha rasmi; hakuna nafasi ya kufundisha wala kutumia Kimakunduchi na wanafunzi wenyewe wanaona lahaja yao kuwa ya hadhi ya chini.

Maelezo hayo yanaonyesha wazi jinsi mfumo wa elimu unavyochangia lahaja hii kupoteza hadhi yake kijamii na kielimu. Kwa mujibu wa *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972), mazingira ya lugha katika elimu yanaathiri sana uhai wa lugha. Nurse na Hinnebusch (1993) pia wanabainisha kwamba lahaja hupungua matumizi yake pale inapokosa nafasi katika mfumo wa elimu. Hivyo, mazingira haya yanachangia kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi, kwani vijana wanaikosa katika mfumo wao wa elimu na hivyo kuiona kama lugha isiyokuwa muhimu kwa maendeleo yao.

Aidha, Kiswahili Sanifu hutazamwa kama chombo muhimu cha maendeleo, hali inayofanya lahaja ya Kimakunduchi kupoteza mvuto wake miongoni mwa vijana. Katika usaili na vijana wa Makunduchi, mmoja wao alisema:

> Kimakunduchi ni lugha ya zamani; haiwezi kutusaidia kupata kazi nzuri wala maendeleo, ndio maana tunapendelea kutumia Kiswahili Sanifu.

Mtazamo huo unadhihirisha namna lahaja hii inavyochukuliwa kama kikwazo kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika uchambuzi wa *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha*, Haugen (1972) anaeleza kuwa thamani ya lugha katika mazingira ya kiuchumi na kijamii huchangia pakubwa katika kuendelea au kufifia kwake. Vile vile, Batibo (2005) anaeleza kuwa lugha zinazotazamwa kuwa na thamani ya chini ya kiuchumi na kijamii hupoteza wazungumzaji wake kwa haraka. Kwa hivyo, kutokana na mtazamo huu wa vijana, Kiswahili Sanifu kimejengewa hadhi kubwa zaidi na kimetambuliwa rasmi kama njia ya kufikia maendeleo na hivyo kuchochea mchakato wa kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi.

***Mabadiliko ya Kijamii na Kizazi***

Vijana wengi wa Makunduchi wameathiriwa na mitazamo ya kimataifa pamoja na mitindo ya maisha ya miji, jambo ambalo limeathiri matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi. Hali hii inatokana na vijana wengi kuvutiwa zaidi na utamaduni na lugha zinazotumika katika miji mikubwa, zikionekana kama alama ya maendeleo ya kisasa. Kijana mmoja kutoka Makunduchi alieleza:

> Tunapenda kutumia Kiswahili Sanifu na Kiingereza zaidi kwa sababu hizo ndiyo lugha za mjini, zinatupa nafasi nzuri ya kuonekana tumesoma na kuwa watu wa kisasa.

Maelezo hayo yanaonyesha kwamba vijana wanathamini zaidi lugha ambazo zinaonekana kuendana na mazingira ya kisasa, jambo ambalo linaathiri vibaya lahaja yao. Kwa mujibu wa Haugen (1972), mabadiliko katika mazingira ya kijamii na kiutamaduni yanaweza kuathiri moja kwa moja lugha, hasa pale inapokosa nafasi ya matumizi mapana katika mazingira mapya. Crystal (2008) anaongeza kuwa lugha zinazohusishwa na maendeleo ya kijamii na kiuchumi huwa na nafasi kubwa zaidi ya kustawi, huku lahaja za kiasili zikididimia. Kwa hivyo, mitazamo hii ya vijana inachangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa matumizi ya Kimakunduchi katika maisha yao ya kila siku.

Aidha, uhamiaji wa ndani pamoja na ndoa mseto umepunguza pakubwa matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi majumbani. Kwa mujibu wa Juma (2019) familia nyingi zinazotokana na ndoa mseto

hujikuta zikilazimika kutumia Kiswahili Sanifu au lugha nyingine zinazokubalika zaidi ili kuhakikisha mawasiliano rahisi kati ya wanandoa na watoto wao. Mama mmoja aliyeolewa na mtu kutoka nje ya Makunduchi alieleza:

> Nyumbani kwetu tunatumia zaidi Kiswahili Sanifu kwa sababu mume wangu hatoki hapa, hivyo hatuwezi kutumia Kimakunduchi mara nyingi.

Maelezo hayo yanaonyesha namna ndoa mseto zinavyopunguza nafasi ya lahaja hii kutumika majumbani, jambo linalopunguza uwezekano wa watoto kuifahamu na kuitumia. *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972) inaeleza kuwa mazingira ya nyumbani ni muhimu kwa uendelevu wa lugha au lahaja yoyote. Fishman (1991) pia anasisitiza umuhimu wa urithishaji wa lugha kupitia matumizi ya nyumbani katika kudumisha lugha. Hivyo basi, uhamiaji wa ndani na ndoa mseto zimechangia kupunguza matumizi ya Kimakunduchi majumbani na hivyo kuiweka lahaja hii katika hatari kubwa ya kutoweka.

Vile vile, mfumo rasmi wa elimu ambao unafundisha watoto kwa kutumia Kiswahili Sanifu au Kiingereza badala ya lahaja za asili umechangia pakubwa katika kufifia kwa Kimakunduchi. Watoto wa Makunduchi hawapati fursa ya kujifunza lahaja yao ya asili wakiwa skuli, hivyo kukosa ujuzi muhimu wa kuitumia katika mazingira rasmi na yasiyo rasmi. Mwalimu mmoja katika skuli ya msingi Makunduchi alisema:

> Sisi tunafundisha kwa Kiswahili Sanifu na Kiingereza pekee; hakuna nafasi kwa Kimakunduchi hata kidogo. Watoto wanakua bila kuifahamu lahaja yao.

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi mfumo wa elimu unavyochangia katika kutokomeza matumizi ya lahaja. Kwa mujibu wa Haugen (1972), mazingira rasmi kama vile skuli yana ushawishi mkubwa katika kuamua hatima ya lugha au lahaja. Batibo (2005) anaongeza kuwa lugha ambayo haipati nafasi katika mifumo ya elimu huwa katika hatari kubwa ya kupotea. Kwa hivyo, kutokana na mazingira haya ya elimu, lahaja ya Kimakunduchi inakosa nafasi ya kukuzwa na kuhifadhiwa, jambo ambalo linaongeza kasi ya kufifia kwake.

***Ukomo wa Matumizi ya Lahaja Katika Maeneo Rasmi***

Lahaja ya Kimakunduchi imepoteza nafasi yake katika maeneo rasmi kama elimu, dini, siasa na biashara, jambo ambalo limeifanya ibaki kutumika katika mazingira machache yasiyo rasmi kama nyumbani na katika hafla za kiutamaduni pekee. Kwa mfano, kiongozi mmoja wa kidini kutoka Makunduchi alisema:

> Katika mawaidha na darsa zetu tunatumia Kiswahili Sanifu pekee; lahaja yetu haitumiki hata kidogo msikitini kwa sababu siyo rasmi.

Maelezo haya yanaonesha wazi kwamba lahaja hii imefungiwa katika mazingira yasiyo rasmi pekee, hali inayopunguza umuhimu wake katika jamii. Kwa mujibu wa Haugen (1972), lugha inahitaji kutumika katika mazingira mbalimbali rasmi ili iweze kudumisha thamani yake na kuendelea kuwepo. Batibo (2005) anaongeza kuwa lugha au lahaja zinazokosa nafasi katika maeneo rasmi ya kijamii hukosa uhai wa kudumu. Hivyo basi, ukosefu huu wa matumizi ya Kimakunduchi katika maeneo rasmi unachangia pakubwa kupunguza matumizi yake na kuiweka katika hatari kubwa ya kutoweka kabisa.

Aidha, kukosekana kwa maandiko rasmi ya kielimu au fasihi katika lahaja ya Kimakunduchi kumechangia kudhoofisha nafasi yake katika jamii. Kutokana na lahaja hii kutokuwa na maandiko kama vile vitabu vya masomo na fasihi zilizoandikwa, wazungumzaji wake hawapati nafasi ya kuisoma wala kuijifunza rasmi. Mwandishi mmoja wa Makunduchi alibainisha:

> Tatizo kubwa ni kwamba hakuna maandiko rasmi kwa Kimakunduchi; hata watoto wetu hawawezi kujifunza kupitia maandishi, hivyo lahaja yetu inazidi kupoteza nafasi yake.

Maelezo hayo yanaonyesha umuhimu wa maandiko katika kuhifadhi na kuimarisha lugha au lahaja yoyote. *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972) inasisitiza umuhimu wa mazingira ya

kielimu na maandiko katika kuendeleza lugha. Crystal (2008) pia anasisitiza kwamba maandiko ni muhimu sana katika kuhakikisha uendelevu wa lugha, kwani huwezesha lugha kurithishwa kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, ukosefu wa maandiko katika Kimakunduchi ni changamoto kubwa inayohitaji kutatuliwa ili kuiokoa lahaja hii kutoka hatari ya kupotea.

***Maendeleo ya Teknolojia na Vyombo vya Habari***

Maendeleo ya teknolojia na matumizi ya vyombo vya habari yamechangia kwa kiasi kikubwa kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na kutumiwa kwa lugha sanifu na za kigeni pekee. Mitandao ya kijamii kama *Facebook, Instagram, WhatsApp* na *Twitter* imejikita zaidi katika matumizi ya Kiswahili Sanifu na Kiingereza. Kijana mmoja kutoka Makunduchi alisema:

> Hatuna namna nyingine, mitandao yote inatumia lugha za kisasa kama Kiswahili Sanifu na Kiingereza; hakuna anayependa kutumia lahaja yetu kwenye mitandao kwani huwezi kueleweka na wengine.

Maelezo hayo yanaonyesha kuwa matumizi ya teknolojia yanamlazimisha mtu kuachana na lahaja yake ya asili ili aweze kushiriki kikamilifu kwenye majukwaa haya ya kisasa. Kwa mujibu wa Haugen (1972), mazingira ya kiteknolojia yana nguvu kubwa katika kuamua hatima ya lugha kutokana na uwezo wake wa kuenea haraka na kufikia watu wengi. Crystal (2008) pia anathibitisha kuwa teknolojia mpya ina mchango mkubwa katika kubadilisha tabia za matumizi ya lugha. Hivyo basi, matumizi ya teknolojia mpya yanaongeza kasi ya kupungua kwa lahaja kama Kimakunduchi, kwani hazina nafasi katika mazingira haya.

Aidha, vijana wengi wanatumia lugha mchanganyiko maarufu kama Kiswanglish katika mawasiliano yao ya kila siku, hasa wanapotumia mitandao ya kijamii au hata katika mazungumzo ya kawaida. Hii imefanya lahaja ya Kimakunduchi kukosa nafasi katika mazungumzo yao. Kijana mmoja alisema:

> Mara nyingi tunachanganya Kiswahili na Kiingereza, ni rahisi na inaonekana vizuri zaidi, hatuna sababu ya kutumia Kimakunduchi.

Maelezo hayo yanaonyesha namna lugha mchanganyiko inavyochukua nafasi ya lahaja za asili katika mawasiliano ya vijana. Kwa mujibu wa *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972), mabadiliko katika matumizi ya lugha yanayoongozwa na vijana yanaweza kuharakisha mchakato wa kupotea kwa lahaja asili ambazo hazitumiki tena katika mazingira hayo mapya. Batibo (2005) pia anaeleza kwamba vijana ndio msingi mkuu wa matumizi ya lugha katika siku zijazo, hivyo wanapoacha kutumia lahaja zao za asili, lugha hizo zinaingia katika hatari kubwa ya kutoweka kabisa.

Vile vile, matumizi ya maneno ya mitindo (slang) ambayo hayatokani na lahaja za asili yamechangia katika kudhoofisha matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi. Vijana wanapendelea kutumia maneno mapya yanayotokana na lugha maarufu kama Kiswahili Sanifu na Kiingereza badala ya kutumia msamiati wa lahaja yao ya asili. Mfano kijana mmoja alitoa maelezo haya:

> Sisi tunatumia maneno ya kisasa kama 'kula bata' na 'piga shoo' badala ya maneno ya Kimakunduchi kwa sababu yanaonekana ya kizamani sana.

Maelezo hayo yanaonyesha kwamba vijana wanaona maneno ya lahaja yao kuwa ya zamani, hivyo kukimbilia matumizi ya misemo mipya yenye mvuto wa kisasa. Haugen (1972) anaeleza kuwa mabadiliko ya msamiati yanayotokana na mitindo mipya katika jamii yanaweza kuathiri sana matumizi ya lahaja za kienyeji. Crystal (2008) anaongeza kuwa maneno ya mitindo yana nguvu kubwa ya kuvutia vijana na hivyo kupunguza nafasi ya maneno ya lahaja. Kwa hivyo, matumizi ya maneno ya mitindo yanachangia katika kupunguza matumizi ya Kimakunduchi na kuongeza kasi ya kupotea kwake.

***Ukosefu wa Mipango ya Kisera ya Kuhifadhi Lahaja***

Ukosefu wa mipango madhubuti ya kisera kutoka serikalini na katika taasisi mbalimbali umechangia kwa kiasi kikubwa kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi. Taasisi za elimu, utamaduni na serikali kuu hazijatunga sera maalumu za kulinda na kukuza lahaja hii, hali inayofanya mazingira ya matumizi yake kuwa magumu zaidi. Kiongozi mmoja wa kijamii kutoka Makunduchi alibainisha:

> Hakuna sera zozote rasmi zinazotambua au kuendeleza lahaja yetu; tunatumia juhudi zetu binafsi tu, lakini haitoshi.

Maelezo hayo yanaonyesha wazi kwamba bila juhudi za kitaasisi na kisera, juhudi binafsi za jamii haziwezi kuwa na mafanikio makubwa katika kuhifadhi lahaja. Haugen (1972), kupitia Nadharia yake ya *Ikolojia ya Lugha*, anaeleza kuwa sera rasmi za lugha ni muhimu sana katika kuweka mazingira yanayostawisha matumizi na maendeleo ya lugha. Aidha, Batibo (2005) anasisitiza umuhimu wa sera za lugha katika kuhakikisha lugha ndogo na lahaja zinapewa nafasi katika jamii. Kwa hivyo, ukosefu wa sera hizi umechangia pakubwa katika kudhoofisha nafasi ya lahaja ya Kimakunduchi na kuifanya iwe katika hatari kubwa ya kupotea kabisa.

Aidha, serikali na taasisi nyingi zimekuwa zikitoa kipaumbele kwa lugha kuu na lugha za kimataifa kama vile Kiswahili Sanifu na Kiingereza, kwa madai kwamba lugha hizo ni muhimu kwa maendeleo na ushirikiano wa kimataifa. Kiongozi mmoja wa elimu huko Makunduchi alisema:

> Tunatoa kipaumbele kwa Kiswahili Sanifu na Kiingereza kwa sababu ni lugha zinazotuwezesha kushiriki katika maendeleo ya kimataifa; hatuoni umuhimu mkubwa wa kutumia rasilimali katika lahaja kama Kimakunduchi.

Mtazamo huo unadhihirisha wazi kwamba lahaja ndogo zinadharauliwa kutokana na dhana kwamba hazina mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Haugen (1972) anaeleza kuwa mtazamo wa kijamii na kisiasa kuhusu thamani ya lugha una athari kubwa katika uhai wake. Crystal (2008) anaongeza kuwa lugha zinazopokea msaada wa sera na rasilimali huwa na uwezo mkubwa wa kustawi. Kwa hivyo, mtazamo huu wa serikali na taasisi kuhusu umuhimu wa lugha kuu pekee unachangia pakubwa katika kupunguza nafasi ya Kimakunduchi katika jamii na kuharakisha kupotea kwake.

***Kuathiriwa kwa Maadili ya Kiutamaduni***

Kufifia kwa mila na desturi za kiutamaduni katika jamii ya Wamakunduchi kumeathiri kwa kiasi kikubwa matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi, kwani lahaja ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote. Mila na desturi za jadi ambazo zilikuwa zikisimamiwa kupitia matumizi ya lahaja hii zimeanza kupotea kutokana na athari za utandawazi na utamaduni wa kigeni. Mzee mmoja kutoka Makunduchi alieleza:

> Miaka ya nyuma tulikuwa tukikusanyika na kutumia Kimakunduchi kwenye hadithi, mashairi na sherehe; siku hizi vijana hawashiriki tena mambo haya, hivyo lahaja yetu inapoteza nafasi yake.

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi mabadiliko ya kiutamaduni yanavyoathiri nafasi ya lahaja katika jamii. Kwa mujibu wa *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972), lugha au lahaja huathiriwa sana na mazingira yake ya kiutamaduni. Mdee (2010) pia anabainisha umuhimu wa mila na desturi katika kuhifadhi lugha na lahaja za asili. Kwa hivyo, kupungua kwa mila na desturi kumechangia kwa kiasi kikubwa kupoteza nafasi ya Kimakunduchi katika maisha ya kila siku ya jamii.

Aidha, sherehe za kiutamaduni kama vile Mwaka Kogwa ambazo zilikuwa zikitoa nafasi muhimu ya kutumia lahaja ya Kimakunduchi zimekuwa zikitumika mara chache, hivyo kupunguza zaidi matumizi ya lahaja hii. Vijana wengi wamekuwa wakipunguza ushiriki wao katika sherehe hizi, wakivutiwa zaidi na matukio mengine ya sasa. Mshiriki mmoja wa sherehe hizi alisema:

> Mwaka Kogwa zamani ilikuwa fursa nzuri sana ya kutumia Kimakunduchi; lakini sasa sherehe hizi hazina umaarufu kama zamani, vijana hawashiriki kwa wingi, hivyo lahaja haitumiki tena ipasavyo, wengine hubakia mjini hawaji kae (kijiji).

Maelezo hayo yanaonyesha kwamba kupungua kwa ushiriki katika sherehe hizi kunapunguza nafasi ya matumizi ya lahaja. Haugen (1972) anasisitiza kuwa mazingira ya utamaduni ni muhimu katika kudumisha lugha au lahaja yoyote, kwani shughuli za kiutamaduni husaidia katika kurithisha lugha kwa vizazi vijavyo. Crystal (2008) anabainisha kuwa matukio ya kiutamaduni ni muhimu kwa uhai wa lugha za asili. Kwa hivyo, kupungua kwa matumizi ya Kimakunduchi katika matukio ya kiutamaduni kama Mwaka Kogwa kunaongeza kasi ya kufifia kwa lahaja hii muhimu.

**Athari za Kufifia kwa Lahaja ya Kimakunduchi**

Kuna athari mbalimbali ambazo zimeanza kujitokeza na zinaendelea kujitokeza kutokana na kuanza kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

Mosi, kupotea kwa maarifa asilia yaliyohifadhiwa katika lahaja ya Kimakunduchi ni athari mojawapo inayotokana na kufifia kwa lahaja hii. Maarifa ya jadi kuhusu mimea ya dawa, kilimo na uvuvi yanaweza kupotea kutokana na vizazi vipya kutofahamu msamiati maalumu wa Kimakunduchi. Mzee mmoja alisema:

> Vijana wetu hawajui tena majina ya mimea na tiba za kienyeji kwa sababu haya yako katika Kimakunduchi tu.

Maelezo hayo yanaonyesha umuhimu wa lahaja katika kuhifadhi maarifa ya asili. Kwa mujibu wa Haugen (1972), lugha ni chombo muhimu cha kuhifadhi maarifa ya kijadi na Crystal (2008) anaongeza kuwa kupotea kwa lugha au lahaja husababisha kupotea kwa maarifa muhimu ya kijamii na kiuchumi.

Pili, kupungua kwa utambulisho wa jamii ya Wamakunduchi ni athari nyingine kubwa. Lahaja kama Kimakunduchi hutambulisha jamii na kutoa hisia za umoja na urithi wa kipekee. Mkazi mmoja alibainisha:

> Lahaja yetu ndiyo inatutambulisha sisi kama Wamakunduchi; bila hiyo, utambulisho wetu unapotea.

Maelezo hayo yanasisitiza umuhimu wa lahaja katika kujenga utambulisho wa jamii. Kwa mujibu wa *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* (Haugen, 1972), lahaja ina uhusiano mkubwa na utambulisho wa kijamii. Mdee (2010) anaongeza kuwa lugha ni msingi wa utambulisho wa jamii yoyote.

Tatu, kuharibika kwa urithi wa fasihi simulizi ni athari nyingine inayotokana na kufifia kwa lahaja hii. Fasihi kama vile hadithi, methali na mashairi ambayo huwasilishwa kwa Kimakunduchi yanaweza kupotea kabisa. Mtoataarifa mmoja alieleza:

> Watoto wetu hawajui tena hadithi za jadi wala methali zetu kwa sababu hawafahamu vizuri lahaja yetu.

Maelezo hayo yanaonyesha umuhimu wa lahaja katika kuendeleza fasihi simulizi. Haugen (1972) anasisitiza kuwa mazingira ya kiutamaduni kama fasihi simulizi ni muhimu kwa uhai wa lugha. Batibo (2005) anaongeza kuwa fasihi simulizi ni muhimu katika kurithisha lugha na utamaduni kwa vizazi vijavyo.

Nne, kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi kunaweza kusababisha mgawanyiko wa kizazi, ambapo wazee na vijana wanashindwa kuwasiliana kwa ufanisi kutokana na tofauti za lugha zinazotumiwa. Mzee mmoja alisema:

> Hatuelewani tena vizuri na wajukuu zetu kwa sababu wao hawajui Kimakunduchi vizuri.

Maelezo hayo yanaonyesha athari ya mgawanyiko wa mawasiliano kati ya vizazi. Kwa mujibu wa Haugen (1972), lugha ni kiungo muhimu kinachounganisha vizazi mbalimbali katika jamii. Fishman (1991) anaeleza umuhimu wa urithishaji wa lugha ili kuzuia mgawanyiko huo wa kizazi.

Tano, kufifia kwa Kimakunduchi kunadhoofisha juhudi za utalii wa kiutamaduni katika eneo la Makunduchi, kwani wageni huvutiwa na utofauti na urithi wa lugha. Mtoa taarifa mmoja ambaye ni anafanya biashara ya utalii alisema:

> Wageni wanapenda kusikia lugha yetu asili, wanapokuta hakuna matumizi ya lahaja yetu tena, wanakosa ile ladha ya kiutamaduni waliyotegemea.

Maelezo hayo yanaonyesha umuhimu wa lahaja katika kukuza utalii wa kiutamaduni. Haugen (1972) anaeleza kuwa mazingira ya kiuchumi, kama utalii, yanaweza kuchangia katika kuhifadhi lugha ikiwa yanathamini lugha hiyo. Crystal (2008) anasisitiza umuhimu wa lugha katika kukuza na kuhifadhi utalii wa kiutamaduni.

**Mapendekezo ya Kuokoa na Kuhuisha Lahaja ya Kimakunduchi**

Baada ya kubaini sababu zinazochangia kufifia kwa lahaja ya Kimakunduchi na kuona athari zilizokwishajitokeza na zile zinazojitokeza, mwandishi wa makala haya anapendekeza zichukuliwe hatua zifuatazo:

Kufanyika utafiti na utunzaji wa maandiko ya lahaja ya Kimakunduchi ni hatua muhimu katika kuilinda lahaja hii isije ikapotea kabisa. Hatua hii inaweza kuhusisha kurekodi sauti za wazungumzaji wenye ufasaha, kukusanya hadithi, methali, misemo na maandiko mengine yanayotumia lahaja hii. Kwa mfano, taasisi kama Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar inaweza kuendesha miradi maalumu ya utafiti na uhifadhi. Haugen (1972) anaeleza kuwa lugha huweza kuhifadhiwa kupitia maandiko rasmi zinazowezesha uhamishaji wake kwa vizazi vijavyo.

Vilevile, mfumo wa elimu unaweza kuwa chombo muhimu cha kuhuisha lahaja hii kwa kujumuisha matumizi yake katika mitaala ya skuli za msingi na sekondari. Skuli zinaweza kuanzisha vipindi maalumu vinavyowezesha wanafunzi kujifunza lahaja kupitia michezo ya kuigiza, mashairi na nyimbo za kienyeji. Kwa mfano, skuli ya msingi Makunduchi inaweza kuanzisha klabu za lugha zinazohamasisha matumizi ya Kimakunduchi. *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972) inaonyesha umuhimu wa mazingira rasmi ya elimu katika ustawi wa lugha yoyote.

Aidha, vyombo vya habari vya kijamii vinaweza kuwa njia nzuri ya kukuza matumizi ya Kimakunduchi kupitia vipindi maalumu kwenye redio na televisheni za kijamii. Vipindi hivi vinaweza kujumuisha mijadala, maigizo na nyimbo za kiutamaduni zinazotumia lahaja hii. Mfano halisi ni redio za jamii kama Makunduchi FM ambazo zinaweza kuanzisha vipindi maalumu vya Kimakunduchi. Kwa mujibu wa Crystal (2008), matumizi ya vyombo vya habari ni njia bora ya kueneza na kuhifadhi lugha au lahaja zilizo katika hatari.

Sherehe za kiutamaduni kama vile Mwaka Kogwa zinaweza kupewa umuhimu zaidi katika juhudi za kuhifadhi Kimakunduchi. Jamii inaweza kuhamasishwa kutumia lahaja yao katika sherehe hizi ili kuhakikisha vijana wanapata fursa ya kujifunza na kuzungumza lahaja hiyo. Kwa mfano, Baraza la Utamaduni Zanzibar linaweza kuanzisha kampeni maalumu za uhamasishaji katika kipindi cha Mwaka Kogwa. Haugen (1972) anabainisha umuhimu wa shughuli za kiutamaduni katika kuhifadhi lugha.

Ushirikiano na wazee wenye ufasaha katika lahaja hii ni njia nyingine muhimu ya kuihuisha lahaja ya Kimakunduchi. Wazee wanaweza kuwa walimu wa kujitolea katika vituo vya kijamii na skuli ili kuwafundisha vijana. Mfano mzuri ni mradi maalumu wa jamii wa Makunduchi ambao unaweza kuanzisha darasa la lahaja likiwa na wazee kama walimu. Fishman (1991) anasisitiza umuhimu wa wazee katika mchakato wa kurithisha lugha kutoka kizazi kimoja kwenda kingine.

Zaidi, jamii inaweza kuandaa mashindano na matamasha ya lugha ambayo yanahamasisha matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi, hivyo kuifanya iwe na mvuto kwa vijana na watu wa rika zote. Kwa mfano, tamasha la lugha la kila mwaka Makunduchi litakuwa njia bora ya kuvutia umma kutumia lahaja hii. Crystal (2008) anaeleza kuwa matamasha ya lugha yana mchango mkubwa katika kukuza utamaduni na lugha za jamii mbalimbali.

Pamoja na hayo, ni muhimu kuandaa machapisho rasmi na vitabu vinavyotumia lahaja hii ili kuongeza uelewa na matumizi yake katika jamii. Machapisho yanaweza kujumuisha hadithi za watoto, vitabu vya fasihi na kamusi. Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar inaweza kuongoza juhudi hizi. Haugen (1972) anasisitiza kuwa maandiko rasmi yanasaidia sana katika kuhifadhi lugha.

Serikali na taasisi za elimu zinapaswa kuandaa sera maalumu zinazolenga kuhuisha na kuhifadhi lahaja ya Kimakunduchi. Sera hizi zinapaswa kutoa mwongozo kuhusu matumizi ya lahaja katika maeneo rasmi kama elimu na vyombo vya habari. Crystal (2008) anabainisha umuhimu wa sera za lugha katika kuhakikisha uhai na maendeleo ya lugha ndogo.

Teknolojia mpya inaweza kutumika kuhuisha matumizi ya Kimakunduchi kupitia programu za simu na mitandao ya kijamii zinazotumia lahaja hii. Vijana wanaweza kuhamasishwa kutumia lahaja katika mawasiliano yao ya kila siku kupitia programu maalumu kama *WhatsApp* au *Facebook*.

Haugen (1972) anaeleza kuwa mazingira ya kiteknolojia yanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uhifadhi wa lugha.

Mwisho, ni muhimu kuimarisha ushirikiano kati ya serikali, jamii na wanataaluma ili kuweka mikakati endelevu ya kuhifadhi na kuhuisha lahaja ya Kimakunduchi. Ushirikiano huu unaweza kujumuisha utafiti wa pamoja, miradi ya jamii na shughuli za elimu zinazolenga lahaja hii. Kwa mujibu wa Batibo (2005), ushirikiano wa wadau mbalimbali ni muhimu sana katika kufanikisha juhudi za kuhifadhi lugha zilizo hatarini.

**Hitimisho**

Lahaja ya Kimakunduchi ni hazina adhimu ya lugha na utamaduni wa jamii ya Zanzibar, hasa watu wa Kusini. Kufifia kwake ni matokeo ya vigezo vya kijamii, kisera, kiutamaduni na kiteknolojia vinavyopaswa kuchunguzwa kwa kina. Hatua madhubuti zinahitajika ili kuhifadhi lahaja hii kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo na kwa kuhifadhi utambulisho wa watu wa Makunduchi. Makala haya yamebainisha kuwa mabadiliko ya kijamii na kizazi, ukosefu wa sera za lugha, matumizi ya Kiswahili Sanifu katika maeneo rasmi na maendeleo ya teknolojia ni sababu kuu zinazochangia kufifia kwa Kimakunduchi. Vijana wa leo wanakosa hamasa ya kutumia lahaja hii kutokana na mtazamo wa jamii unaohusisha lahaja na ujinga au usasa wa zamani. Kutotumika kwa Kimakunduchi katika elimu, vyombo vya habari na nyanja nyingine rasmi kumeifanya lahaja hii kushindwa kushindana na lugha nyingine zenye ushawishi mkubwa.

Kwa kutumia *Nadharia ya Ikolojia ya Lugha* ya Haugen (1972), makala imeonyesha kuwa lugha au lahaja inaweza kufifia iwapo mazingira yanayozunguka matumizi yake hayaiungi mkono. Kimakunduchi kimekosa uungwaji mkono wa kisera, kiteknolojia na kijamii, hali inayosababisha kudorora kwa matumizi yake. Vile vile, kupungua kwa matumizi ya lahaja hii kumechangia kupotea kwa maarifa ya asili, fasihi simulizi na kutetereka kwa utambulisho wa jamii ya Wamakunduchi. Ili kuzuia hali hii kuendelea, kuna haja ya kuweka mikakati ya utafiti, elimu, matumizi ya teknolojia, ushirikiano na wazee wa jamii na matumizi ya lahaja katika maadhimisho ya kiutamaduni. Serikali, taasisi za elimu, wanataaluma na jamii kwa ujumla wanapaswa kushirikiana kwa karibu kuhakikisha kuwa Kimakunduchi si tu inahifadhiwa, bali pia inahuishwa na kuendelezwa kwa msingi wa heshima, elimu na urithi wa kizalendo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumelinda si tu lugha, bali pia roho ya utamaduni wa jamii ya Wamakunduchi.

**Marejeo**

Batibo, H. M. (2005). *Language decline and death in Africa: Causes, consequences and challenges*. Multilingual Matters.

Crystal, D. (2008). *Language death*. Cambridge University Press.

Fishman, J. A. (1991). *Reversing language shift: Theoretical and empirical foundations of assistance to threatened languages*. Multilingual Matters.

Haugen, E. (1972). *The ecology of language*. Stanford University Press.

Iddi, Z.A. (2011). Phonological Processes in Kimakunduchi Dialect. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Iddi, Z.A. (2018). Ulinganishi wa Kiisimu wa Kitumbatu na Kimakunduchi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Juma, H.K. (2019). Ulinganishi wa Kihistoria na Kiisimu wa Lahaja za Kiamu, Kimvita, Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B. (2017). *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya.* Kiswahili Development Limited.

Mazrui, A. M. & Mazrui, A. A. (1995). *Swahili state and society: The political economy of an African language*. East African Educational Publishers.

Mdee, J. S. (2010). *Fasihi simulizi na uhifadhi wa lugha za Kiafrika*. TUKI Working Papers, University of Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (2002). Development of Kiswahili as a national and official language: The case of Tanzania. In *Language and Development in Africa*.

Nurse, D. & Hinnebusch, T. J. (1993). *Swahili and Sabaki: A linguistic history*. University of California Press.

Qorro, M. A. S. (2009). Parents' and policy makers' insistence on foreign languages as media of education in Africa: Restricting access to quality education – for whose benefit? In B. Brock-Utne & I. Skattum (Eds.), *Languages and education in Africa: A comparative and transdisciplinary analysis* (pp. 31–48). Symposium Books.

UNESCO. (2003). *Language vitality and endangerment*. UNESCO Ad Hoc Expert Group on Endangered Languages.